Maisha ya Jumuiya

Christian Patzl, SDS

15 June, 2016

Utangulizi

Kama Wasalvatoriani tupo na tunajisikia kuunganika kwa njia mbalimbali, hasa kupitia wazo la mwanzilishi wetu, Pd. Jordani. Maisha yetu ya Kisalvatoriani yamejengwa katika maisha ya jumuiya. Tunahitaji msingi huu kama chanzo cha maisha yetu ya Kisalvatoriani ambayo tunachota nguvu mpya na mawazo mapya na ambapo tunachota kutoka kwa Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, ni muhimu kuboresha na kukuza jumuiya hii.

Kila jina katika haya matawi matatu ambayo yamejiunga chini ya paa la familia ya Kisalvatoriani inatafakari namna ya maisha yaliyochaguliwa na wanachama wake: Jumuiya. Laikini jumuiya hii inaonekanaje kwa maneno ya uhalisia na itawezaje kutafuta namna ya kuonekana ndani ya familia ya Kisalvatoriani? Uangalizi wa pekee huonyesha kwamba matawi yote matatu yana jumuiya ambazo zinafanya kazi kwa namna moja au nyingine. Kwa sababu hakuna kazi inayoonyesha juu ya somo hili mpaka sasa, ni muda mwafaka wa kuchimba juu ya swala la maisha ya jumuiya katika kiwango cha juu, na zaidi ya yote kwa sababu sheria ya familia ya wasalvatoriani[1] inatupa changamoto kuishi maisha kama jumuiya inayopendana.

Katika kila tawi, jumuiya zimeanzishwa tofauti na kwa hali zinazotofautiana. Kwa Wasalvatoriani[a] walei imekuwa ni kawaida kwamba kundi hili lilianza na Padre Msalvatoriani au Sista Msalvatoriani. Malezi ya Kisalvatoriani ndio swala la msingi katika hatua ya kujenga jumuiya zaidi ya hapo, mahitaji ya wanachama hayakuangaliwa kwa umakini mkubwa au hayakuangaliwa kabisa, ingawa mahitaji haya yana mchango mkubwa sana katika maendeleo ya jumuiya ya kweli. Kuna sababu nyingi zinazosababisha mambo haya, kuanzia nguvu za ziada zinazohitajika kwa kuliwezesha na pia muda uliopo, na pia ukosefu wa uzoefu katika kuliongoza kundi au, kwa kuelewa tu umuhimu wa kuwa na viongozi kati ya wale wanaopenda. Maisha ya kila siku kama tunavyoona katika hali maalum mara zote yanatofautiana kati ya wale wenye daraja na walei – kama ilivyo uelewa ambao kila mmoja anao juu ya njia ya maisha ya wengine.

Kwa hiyo tunawezaje kuona maisha ya jumuiya katika kila tawi na katika familia nzima kwa ujumla? Tunaweza kuanza kwa kujifunza juu ya maana ya jumuiya, jamii na kundi.

Jumuiya ni Nini?

Injili ya Matayo 18:20 tunasoma: *"walipo wawili au watatu wamekusanyika kwa jina langu, Mimi nipo kati yao." Hii tayari inaonyesha wazo la msingi la Jumuiya (ya Kikristo) (au jamii; angalia chini). Kwa hiyo inahusisha watu wenye mawazo yanayofanana na wa kitu ambacho wanacho kwa pamoja. Watu hawa wana aina ya ukaribu wa hisia au, kama wengine wanavyoweza kusema kwa kawaida, wapo katika urefu wa mawimbi yanayolingana. Wanatengeneza uhusiano wa kindugu na wa karibu. Hii ni tafanusi ya elimu jamii ya Jumuiya.*[2] Kwa ujumla, jumuiya ni neno linalo changanya ambalo linaonyesha uhusiano wa pande mbili wa watu ambao wanashiriki kwa

a Kama nijuavyo kuanzishwa kwa jumuiya za Wasalvatoriani Walei kwa undani ningependa kuziangalia kama mfano ulinganifu na jumuiya bila kutofautisha na jumuiya mbili za Kisalvatoriani zilizobaki.

pamoja malengo ya kidini, muono wa ulimwengu, fikra za kisiasa au fikra za kiitikadi, maadili ya kiroho au baadhi ya malelngo machache yanayotekelezeka kama msingi wa pamoja, ambao umefanyika kwa kipindi fulani.[3]

Sheria za maisha ya mwanzo za jumuiya za Kimonaki walikuwa pia na lengo la kutimiza matakwa ya kiinjili kwa kulinganisha Sala na Kazi ("Ora et Labora") na kulihitajika jumuiya yenye maisha safi naya kindugu.[4]

Tunapotafiti juu ya sababu za, au kuhusu kitu kinachounganisha jumuiya, huwa hakuna jibu rahisi kuelewa kwa watu kutoka nje. Kazi mbalimbali[5] zinaonyesha kwamba sababu za kujiunga na jumuiya ni ngumu sana kuzichunguza, lakini sababu kubwa ipo katika lengo la muda mrefu wa kutimiza malengo ya kihisia na tamaa.

Alama zilizo nyoofu za kutokea kwa jumuiya ni muungano unaokuwa kati ya wanachama na matokeo ya uhusiano wao wa karibu. Kwa hiyo, hakuna mgongano wa masilahi katika jumuiya za kweli. Bali, wanachama wanajitahidi kufikia maafikiano, ambayo ni kusema kwamba wanajaribu kushirikishana kwa pamoja juu ya imani, maadili na desturi.

Tofauti kati ya Jumuiya na Jamii

Kama inavyotofautiana na jumuiya, muungano wa watu katika jamii ambao umejikita katika mtazamo wa ufahamu katika jamii ya watu mbalimbali wanaofaidishana ili kuweza kufikia lengo moja. Lengo lipo katika kubadilishana huduma na malipo – kwa hiyo tungeweza kuongelea "jumuiya inayotafuta faida" au kundi katika mtandao wa jamii ya watu ambao wanaelezewa na muunganiko wa wanachama wake.[6]

Kwa hiyo sasa, nini maana ya kundi?

Kwa kawaida kundi huwa na watu kati ya watatu (3) mpaka wasiozidi 25. Watu hawa wana lengo moja la kundi, ambalo linawapa motisha ya tabia zao. Kundi linakuwa na tabia ya kujisikia "usisi." Hii ina maana kwamba wanachama wote wa kikundi wanajiona kama sehemu ya kundi lote na wanafanya kazi kwa kufuatana na mtindo huo.

Kila jumuiya ina mfumo wake wa mila na desturi zinazowasaidia kufikia malengo ya pamoja ya kundi. Mila za msingi zinasababisha tabia za wanakundi ambazo wanazipata kutoka katika desturi hizi.

Kundi pia lina tabia ya mgawanyo wa majukumu ambayo yanarahisisha kufikia malengo ya kundi. Ingawa kuna kujisikia "usisi" katika kundi, kuna umbali fulani uliopo kati ya wanakundi. Katika hali mwafaka wa kweli bado hauhitajiki.

Mwanzo wa Kundi ni Kuonyesha Tabia za Jumuiya

Kundi linaweza likawa na tabia ya Jumuiya, kwa mfano, wakati wanakundi wanakuwa na tabia ya ujirani na wanajaribu kufikia makubaliano wanapofanya maamuzi. Wote wanajisikia "nyumbani" na wanajisikia faraja katika kuepuka migongano ya namna yoyote katika kundi.

Kundi kama hilo lina watu ambao wanafahamiana kwa kipindi kirefu. Mtu mpya anapojiunga na kundi (hata kama ni kwa muda) au pale wengine wanapoliacha kundi, muundo wa kundi unaharibiwa. Jambo hili linawaathiri kila mwana kundi. Mara kwa mara kiwango cha uhusiano na uwazi katika kundi unapungua.

Hatua Nne za Kutengeneza Jumuiya

Sasa ngoja tuone utaratibu wa kutengeneza kundi kwa sababu kundi halitengenezwi kwa usiku mmoja bali unapitia hatua mbalimbali. Kielelezo cha 1 kinaonyesha hatua nne za kutengeneza jumuiya kama ilivyoelezwa na Morgan Scott Peck ambaye ni mwanasaikolojia kutoka America kwa ujumla kila jumuiya inaweza ikawekwa katika moja ya hatua hizi.[b7] Mabadiliko yanatokea lakini yanatofautishwa na sifa za kitabia.

1) Hatua ya Jumuiya – Bandia

Jumuiya zote na makundi yote huanza kukua kwa mtindo huu – na kila mmoja anajua kwamba hatua hii si ya muhimu "porojo" kundi linajifanya kama tayari limekuwa jumuiya, kana kwamba kuna tofauti ndogo sana kati ya wanajumuiya wake na lala hakuna sababu ya migongano. Hali hii, inadumishwa kwa njia ya "Adabu Njema": mengi yanavumiliwa na/au mambo yanayoudhi "yanavumiliwa" ili kuepuka makwazo yanayoweza kutokea; haitakiwi kumuudhi mwanakundi au kumtendea kwa ukatili. "migongano" inatatuliwa kwa tabasamu. Kunapoonekana kuna hatari wanakundi wanabadili mada haraka iwezekanavyo.

- **Hatua ya Jumuiya Bandia**
  - Kujifanya kuna Amani; Jaribio la kustaarabisha
- **Hatua ya Fujo**
  - Migongano ya kudumu, upinzani, Hasira na maumivu, Kutokueleweka.
- **Hatua ya Kujivua**
  - Kukosa Usalama (maumivu), Maongezi kati ya wanakundi Kuhusu wao na mahitaji yao
- **Hatua ya Uhalisia**
  - Moyo wa nguvu moja Unaundwa, na upendo bila Kuwa na sababu.

Hali ya "ulimwengu uliokamilika" inatawala: kila mtu anajitahidi kushiriki na palw inapowezekana anakuwa makini na anayejali wengine. Mara nyingi huwa hakuna maonezi ya kina au majadiliano na kama yapo, yanawekwa katika hali ya chini mno- kama vile yasiyojihusisha na upande wowote, ya heshima, ya kinafiki, ya kuchosha, yasiyo na matunda na yasiyoleta maendeleo – inawaletea mazingira ya wanakundi kujitenga na kundi kwa urahisi.

Hakuna tabaka ya madaraka; kuna uwezekano wa kushirikishana majukumu, lakini huwa inatokea kwa kiwango kidogo sana. Lakini, ushirikishanaji wa majukumu katika hatua hii yasichanganywe kabisa na msaada au utashi wa kusaidia ambao unafanywa kwa kujipendekeza au kwa ajili ya kudumisha amani.

[b] kuna mtindo huo unaoonyeshwa kama mtindo wa "kufanya, kugombana, kuweka sheria na kutekeleza – na B. Tuckman, ila mfumo wake umejikita katika maswala ya uongozi na utawala.

2) Hatua ya Fujo

Baada ya muda fulani hivi, kundi linafikia hali ambayo kiwango cha uvumilivu wa wanachama inapungua. Uimara na udhaifu wa kila mwanakundi unaonekana kwa uwazi sana – ambao kwa muda fulani utaleta migongano. Mambo haya hayafanyiki tena kwa kificho, lakini yanahitaji kuanzishwa. Wanachama wanaanza kuwa na mabadiliko au kuponyeshana; wanahusiana pamoja au/na kujitenga na wengine. Kila wakati kunakuwa na migongano – kujitetea, hasira, ukatili na kutokueleweka inakuwa ni taratibu ya siku, ambayo ikiambatana na kupigania madaraka na kundi linaanza kutengeneza sheria. Kwa nadharia kinachotakiwa ni kushinda au kupoteza na baadhi ya makundi yanaanguka na kurudi katika hatua ya kwanza. Kama kundi hili likivumilia licha ya haya matatizo bila ya kuharibika au kurudi kwenye hatua ya kwanza ya jumuiya – Bandia itakuwa na kuingia katika hatua ya kujivua.

3) Hatua ya Kujivua

Mabadiliko kutoka fujo kuelekea kujivua ni mara chache mno kuwa ya kuigiza. Kinyume chake kabisa, mara nyingi inachukua muda mrefu sana. Hatua hii ya kujivua ni hatua ambayo inahitaji jitihada za pekee. Ni muda ambapo wanachama wanajitahidi kuondoa vikwazo kati yao na katika jumuiya. Wanatambua maumivu ya kila mmoja na wanaelewa umuhimu wa kuongea juu ya mahitaji yao. Uthubutu na ujasiri unahitajika sasa, ingawa wanachama mara zote wanajisikia kusaidiwa, na mara kwa mara wanajisikia wanyonge. Sababu ni kwamba mambo wanayotakiwa kuyaacha na kuyatolea sadaka pamoja na ukamilifu wao ni tabia za ujumla za watu wote: chuki, maamuzi ya kitoto kuhusu ukweli; matarajio yasiyobadilika, na tamaa ya kukuza "itikadi yake na mwono wa ulimwengu; hamu ya kushinda, woga wa kujifanya mpumbavu, na hitaji la kujitawala kila wakati. Kunaweza kuwa kuna mambo ya kipekee kama vile malalamiko ya siri, maudhi au hofu kubwa ya maumivu au udogo wa muhusika mwenyewe.

Mwishowe ujasiri unafuatia na wanachama wanaanza kuongea kwa uwazi na bila kuwajibika kimaadili. Unafika wakati ambapo mwanakundi kwa uhalisi na uhakika anaweza kupambana na jambo bila ya mtu kuona haja ya kubadili mada. Kundi linasikiliza kwa ukimya na kuyachukua yote. Mwanachama mmoja atachukua kwa uangalifu mlolongo mzima, halafu atatoa maoni kwa yale yaliyosemwa au atawasilisha jambo jingine mwafaka. Badala ya hitaji la kuepukana na "utupu" kuna heshima inayokuwa kwa sababu mtu wa pili anamfuata wa kwanza. Kama watu wengine watafuata njia hiyo hatua itakuwa imekamilika – jumuiya itakuwa imeanzishwa katika hali mbalimbali, huu ni muda mwafaka wa maamuzi ambao utashikiliwa na wanakundi wote: inaonekana kana kwamba roho ya amani na faraja inashuka kwa kila mwanakundi.

4) Hatua ya Uhalisia

Kwa dakika moja tu kila kitu kinabadilika. Uaminifu na upendo halisi vinatawala. Udhaifu na madhara yatokanayo yanavumiliwa kwa staha. Wanakundi wanafahamu maeneo ambayo kila mmoja hatakiwi kwenda, ambayo wanayaheshimu na kuingia kwa uangalifu unaostahili wakitenda kwa umakini mkubwa. Mwanakundi juu ya nafasi ya kila mmoja. Watu wanafanya kazi kwa kujali muda kama mziki unaochezwa ukiongozwa na mwimbishaji wa mbinguni asiyeonekana. Wengi wao wanahisi uwepo wa Mungu katika chumba na katika muungano wao.

Lakini sasa, tahadhari inahitajika! Hatua hii haiji kwa bahati mbaya na kuendelea kuwepo, inahitaji kuwajibika sana. Kama vitu vikiachwa vyenyewe au visipopewa uangalizi wa pekee – mfano, mikutano inayoendeshwa kiholela, bila maandalizi ya kutosha, ujio wa wanachama wapya, N.K. –

kundi litaanguka na kurudi katika hatua ya pili na litahitaji kufanya kazi ya ziada na kuanza upya tena.

Mpaka kufikia hatua hii kila kundi – au - jumuiya – ijiulize kama wanachama wake tayari ni "wa moyo na roho moja" kama inavyoonyeshwa katika Matendo ya Mitume 4:32-35 katika maandiko matakatifu:

- *Kwa pamoja kwa mapendo na uaminifu – yaani kuwa na moyo na roho moja.*
- *Kuwa na wito wa kutangaza injili katika kiini cha jumuiya zao.*
- *Kuwa na utumishi wa mapendo – kama jumuiya yenye mali.*

Na kwa hiyo wamefikia hatua ya nne (4), au inawezekana wapo katika moja ya hatua tatu (3) zilizoonyeshwa hapo juu. Lakini usiogope kama ukijikuta upo katika hatua ya pili au hatua ya kwanza kabisa – cha muhimu ni kuelewa utaratibu, kuuchukua na kukubaliana na changamoto.

Lakini wapi pa Kuanzia …?

Kuishi na kuwa pamoja katika jumuiya kunahitaji unyoofu na uaminifu. Kabla ya kutoa hitimisho linalotakiwa, inabidi tuangalie wapi tulipo, na halafu tufanye maamuzi sahihi na kupiga hatua mbele ili kuwa jumuiya ya kweli. Mwanzoni kabisa tunatakiwa kufikiri juu ya mtu gani kumkabidhi ili aweze kulisaidia kundi[c] kwa sababu ushawishi na maamuzi ya mtu huyo ni ya muhimu sana kwa maendeleo ya kundi. Kwa jumuiya ya Mungu Mwokozi wajibu huu mara zote huwa kwa Masista na Mabruda/Mapadre. Kwa kipindi kijacho Wasalvatoriani Walei wanatakiwa kuchukua wajibu huu wao wenyewe kama tunataka jumuiya yao iwe yenye uhalisia na mamlaka ya kweli.[d]

Mtu anayekabidhiwa kuliongoza kundi ni lazima awe na uzoefu wa maisha ya kijumuiya ya Wasalvatoriani kwa miaka kadhaa na ikiwezekana anatakiwa awe ameishi katika makundi/jumuiya mbalimbali. Mtu huyu ni lazima awe mkomavu, kama vile kufanya kazi na watu na kuwa tayari kuwa na uzoefu mpya.

Familia ya Kisalvatoriani ni jumuiya ya kiroho lakini si hivi tu! Maelezo: "mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila neno litokalo kinywani mwa Mungu." (Mt 4:4) inaweza kutupa hali iliyo chanya. Kwa mfano, kama kundi linakutana mara moja tu kwa mwezi kwa muda mfupi wa sala na/au kushirikishana ujumbe wa Biblia, haiwezekani hata siku moja kuwa jumuiya ya kweli. Habaki tu katika hatua ya kwanza; majadiliano yao, na maongezi yao, na kuishi kwao pamoja hauwezi ukakua katika kiwango cha juu. Kwa hiyo kundi linatakiwa kutafuta mambo yatakayowaunganisha na yatakayowavutia ambayo yanaweza yakawa ni ya kiulimwengu kabisa. Kundi linaweza likawa na moyo wa mapishi, katika kazi ya mikono, katika michezo au utamaduni, n.k. chochote watakacho kuwa nacho, jambo la muhimu ni kwa ajili ya wanachama kutafuta msingi wa pamoja katika "maisha ya kawaida." Wajibu muhimu sana katika kuliongoza kundi lipo katika maamuzi ya hatua hii muhimu ya kuwa jumuiya na kutawala utekelezaji wake. Upinzani unawezekana ukawepo juu ya madhara kwa mfano, sasa au baadae kundi linaweza kujikita na mambo ya ulimwengu, kutegemea mtu anayeongoza kundi na pia motisha ya mara kwa mara ya kundi lenyewe.

---

[c] Hii inamaanisha mtu ambaye atawajibika kwa jumuiya husika.
[d] Pia ni hitaji linalohitajiwa kwa ajili ya kuthibitishwa na Roma.

Matukio na kazi ya pamoja linaipa kundi muundo na kuonyesha ubora na madhaifu ya wanachama wake. Udhaifu si lazima uwe ni hasara kila wakati; kundi ni lazima kila wakati lipewe changamoto za kutafuta na kutengeneza masuluhisho kwa pamoja. Shughuli za mapumziko ya pamoja, hija, kutembea umbali mrefu na Biblia, kufanya mafunzo, n.k. inakuza maana ya jumuiya na kukuza hatua za maendeleo ya kundi[e].

Jambo jingine ni kuangalia haiba na nafsi ya kila mmoja katika kundi. Kama mambo haya yakigawanyika vema katika kundi, itafanya maisha kuwa "rahisi" katika kundi. Kwa hiyo si swala la kutojali kuamua watu gani wanatakiwa wajiunge na kundi. Swala hili linahitaji uangalifu. Bali pia katika baadhi ya mambo hata jambo hili halisaidii na magumu huanza kuongezeka. Mtu ambaye si mtaalamu wa mambo ya kijamii hawezi kuwa na furaha katika familia ya Kisalvatoriani kwa kipindi kirefu, na kinyume chake. Hii itazuia maendeleo ya jumuiya ya kweli na kundi linaweza kwa bahati mbaya kuishia katika hatua ya migogoro – ambayo kwa hakika si hali inayotakiwa.

Kwa hiyo, kundi linahitaji uangalizi mzuri wa timu ya Waratibu au viongozi wa kizio watahitaji kubadili muundo wa makundi kwa ajili ya faida ya jumuiya; au, kwa hali fulani, baadhi ya watu inabidi wafukuzwe. Haishangazi kila mara kwamba jambo hili huwa ni changamoto, hasa kwa mtu anayeongoza kundi. Maendeleo ya kundi ni safari – lakini pia kila wakati ni matembezi ya pamoja na Mungu – ambacho ni kitu tunachokitegemea.

Swala la Sehemu na Mtazamo[8]

Kwa jumuiya za kimataifa, uangalizi maalumu ni lazima kutolewa kwa tofauti za mtazamo na pia katika sehemu. Aina ya jambo, kwa mfano, ambalo halionyeshi tatizo lolote kwa mazingira ya Magharibi inaweza ikasababisha mtafaruku mkubwa katika mazingira ya Kiasia au Kiafrika na kinyume chake. Binadamu huwa hawafanani, si kwa muonekano wala kwa namna wanavyohisi.

Kwa hiyo itawezekanaje kujenga jumuiya ya (kweli) ya kimataifa? Jambo hili kwa kweli, zaidi ya yote linahitaji uvumilivu mkubwa, uelewa wa tofauti ya maisha na mazingira, na pia umuhimu wa kukubaliana. Wazo la msingi sit tu kukubali kila kitu, bali kufikia kiwango fulani cha makubaliano. Kama Wasalvatoriani Wanaume na Wasalvatoriani Wanawake tunapata msaada katika ukumbakumba wetu[9]. Ambao unategemea falsafa ya maisha ya Ukiristo wa Kikatoliki[10] na tamaa yetu ya kujifunza kumwamini Mungu na kuruhusu kutajirishwa na ndugu zetu wageni. Kama tukifanikiwa kutoa watu wengi inavyowezekana, fursa ya kuelewa thamani na nafasi ya jumuiya hiyo, kazi kubwa inaweza kutokea, kama ilivyokusudiwa na kufunuliwa na Baba Jordani[f].

Kuishi katika Jumuiya – kwa mambo makubwa na madogo

Kama maisha ya "kundi dogo" kama linafanya shughuli tu, ni muda unaotupasa kuangalia nje ya "mipaka" yetu. Kizio cha nchi au mkoa ni lazima pia ijitahidi kuishi kama jumuiya ya kweli.

Kama nilivyosema hapo juu, shughuli mbalimbali zinaweza kusaidia kufanya na kutunza hisia za "usisi" (umoja). Ni jukumu la timu za kuratibu au kuongoza kutoa mambo muhimu yanayohitajika. Nje ya mikutano mikubwa ya kawaida, matukio ya kielimu, mafunzo, ugunduzi au miradi yanaweza yakafaa.[11] Walau kuwe kuna miradi ya familia ya Kisalvatoriani kwa ushirikiano wa

[e] Kukua kwa kundi kuna maanisha muunganiko na mahusiano ya pamoja kati ya wanachama wa kundi. Inaelezea tabia ya kila mmoja katika kundi, malezi ya kundi na jinsi kundi linavyofanya kazi.
[f] Angalia, Sheria ya Familia ya Wasalvatoriani, Suraya 1 aya ya 2

pamoja na baadhi ya makundi au wanachama wa matawi. Baadhi ya miradi hii na shughuli ingeweza kuchukua sura ya kimataifa.[g]

Je tunaweza Kustahimili Nini?

Hili ni swali ambalo linatakiwa kuulizwa kwa mtu mmojammoja na pia jumuiya ndogo au jumuiya kubwa. Sababu za kuhitilafiana inaweza kuwa matukio ya ghafla kama kifo, ugonjwa (mkubwa) wa mwanachama, rufaa za mara kwa mara kutoka nje, njama na mambo mengine mengi; pamoja pia na mabadiliko yanayojitokeza, yote haya kwa pamoja yanaweka vikwazo katika muundo wa jumuiya.

Uzoefu unaonyesha kwamba jumuiya zenye watu wachache zina uwezo mdogo sana wa kutatua changamoto hizo kuliko jumuiya kubwa. Kwa maneno mengine, kuna "mlolongo mkubwa" ambapo chini yake "tatizo" linageuka kuwa changamoto halisi – mara nyingine inapelekea pia kuvunjika kwa jumuiya.

Idadi kubwa ya watu au namba kubwa ya kundi mojamoja ambazo zipo katika jumuiya zinaleta mgawanyo mzuri. Wanakundi ambao hawajisikii nyumbani katika kundi moja wanaweza wakahamia kwenye kundi jingine. Msemo "kushirikiana tatizo kwa pamoja ni kutatua nusu nzima ya tatizo lote" linaweza likawa na matumizi ya kweli katika mazingira haya, kwa kuwa, watu wengi wanaposhirikishana "tatizo" kila mtu anahisi tatizo hilo kwa uzito mdogo kuliko katika kundi dogo. Hapa, na pia ni juu ya kiongozi wa kundi, timu inayoratibu au timu ya uongozi itafute utatuzi wa matatizo kadri inavyowezekana. Zaidi ya hayo, kila mmoja anakabiliwa na hili swali la msingi:

Je, Ninaweza kuishi maisha ya Jumuiya – au hapana?

Uwezo wa kijamii wa wanachama ni hitaji la msingi kwa kila kundi au jumuiya ambayo inatafuta kuwa na uhusiano mkubwa, au kwa maneno mengine jumuiya inayotaka kuwa thabiti. Kwauhakika kila mmoja atakuwa tayari na vigezo vichache. Wakati haya yote yakiunganishwa itakuwa dhahiri kwa haraka ambapo tofauti zilizopo zitahitajika kuelekezwa nyuma ya jumuiya ya kweli. Yafuatayo ni mambo ya msingi tunayoanza nayo, bila kuwa na deni la ukamilisho wao:

- Je, nina utayari na ukubali wa kutosha kwa mambo tunayoshiriki katika jumuiya?
- Je, ningependa kujihusisha mwenyewe katika jumuiya au ninataka tu kuwa kati ya kundi?
- Je, nipo tayari kujitolea kwa ajili ya wanachama wengine katika jumuiya, kujitoa kwao (bila masharti)?
- Sibagui wengine, bali ninajitenga mwenyewe bila kujua kwa sababu sitaki kuwa sehemu ya kundi au kwa sababu bado sitaki kujihusisha na kundi?
- Je, lengo langu ni kubaki imara katika jumuiya licha ya maafa, migongano na mida isiyo na raha?
- Je, nipo tayari kulinganisha uhuru wangu wa msingi, utu wangu ili kuacha nafasi kwa ajili ya watu wengine/uzoefu mwingine?

[g] Baadhi ya mifano inayowezekana ni miradi ya pamoja ya jamii kati ya mapadre na masista au taasisi zake (→SOFIA, n.k) ambayo tayari inafanya kazi.

Kwa hiyo ni muhimu kwetu kujiangalia mara kwa mara katika kioo sura zetu zilizofubaa na kuchunguza utashi wetu wa kujifahamu na kujisahihisha. Je, ninafanikiwa kutengeneza mazingira ambayo yanawapa wengine uhuru wa kuwa kama walivyo na kuweka wazi hisia zao za kweli? Hii inagonga moja ya sentensi ya Padri Bonaventure Luthen, SDS, ambayo ingekuwa sahihi sana katika mazingira ya uhusiano na jumuiya na ambayo ingeweza kuwa msemo wa kila jumuiya ya Kisalvatoriani: "kukutana nawe."

Jumuiya ya kweli – au Jumuiya ya lengo fulani tu

Tukiangalia jumuiya za kitawa za sasa na za zamani, tunagundua kwamba jumuiya ni nguzo ya kila maisha ya kiroho ya kila jumuiya hizo. Ni mbebaji halisi wa mapokeo ya kitawa na mtindo wa kitawa.[12] Kwa hiyo, jumuiya ina kazi muhimu sana na ni moja kati y nguzo kubwa ya jumuiya kama hizo za watu wenye mawazo yanayofanana. Bila shaka, hii inaonyesha zaidi juu ya jumuiya za kiroho, lakini hata hapa tafanusi inaeleza:

> *Jumuiya ya kitawa ni kikundi cha watu katika Kanisa Katoliki la Roma ambao wanaishi imani yao kwa namna ya asili yao wenyewe. Hii ina maana kwa mfano kama karama pekee kama uhuru au jumuiya ni muhimu, kama vile mtakatifu fulani amechukua sehemu muhimu au kuna utamaduni wa pekee wa sala ili kukomaza muelekeo wa utawa.*[13]

Hii inaoneshwa kwamba jumuiya ya kweli ni kitu ambacho tunahitaji na ulazima kufanya jitihada kwa ajili hiyo – iwe katika vizio vikubwa au vidogo.[h]

Kwa hiyo, jumuiya zetu za Kisalvatoriani ni lazima kwa uwazi, zijitofautishe na vyama vingine kama vile vikundi vya parokia au makundui yaliyo katika mazingira kama hayo. Mengi ya makundi kama haya yana muelekeo wa kuwa jumuiya za malengo fulani na lengo lao la msingi si kuishi pamoja kama ndugu. Kwa hiyo, ingawa wanachama wanaheshimiana na baadhi wanaweza wakaungana kama marafiki, hawahitajiki kupendana mno kwa kupindukia. Mwisho, ni ujumbe kutoka *Gaudium et Spes* ambao unatuonyesha njia: Mungu, ambae ana mapendo ya Kibaba kwa kila mmoja, alipenda kwamba watu wote lazima waunde familia moja na watendeane kwa roho ya mapendo. Kwa kuwa wameumbwa kwa sura na mfano wa Mungu, ambaye "kutoka kwa mtu mmoja aliumba jamii nzima ya watu na kuwafanya waishi juu ya uso wa dunia nzima" (MDO 17:26), watu wote wanaitwa kuwa na lengo moja, ambalo ni Mungu mwenyewe.[14]

Hata kama bado hatuna jumuiya za kweli katika vizio vyetu tunatakiwa tusikate tama au hata kuviua kabisa. Ila, ni lazima tukubali changamoto na kuliweka kuwa lengo letu la kati au la mbali.[i]

Mbali sana – Lakini Karibu sana…

Ulimwengu wetu wa sasa una njia mbalimbali za kisasa za mawasiliano. TV, Redio, na intaneti ambazo zinasaidia maisha ya kila siku katika sehemu mbalimbali za ulimwengu na watu wanaona ugumu kuishi bila hayo. Hata katika maeneo ya mbali sana[15] simu za mikononi zinapatikana na watu wanatumia mitandao ya kijamii kuwasiliana. Zaidi ya yote intaneti inatoa njia mbalimbali kutengeneza mawasiliano na watu wengine, hata kuvuka umbali mkubwa, na kutengeneza mifumo mipya ya jumuiya.

---

[h] Angalia sehemu ya juu: "lakini tuanzie wapi…?"
[i] Angalia, Sheria ya familia ya Wasalvatoriani, sura ivff.

Jukwaa kwa Intaneti, Blogu, simu za kuona & Mambo kama hayo

Vifaa hivi ni vyombo vinavyowaruhusu watu kufanya mawasiliano na mfululizo wa habari kuvuka nchi na mabara.

Jukwaa kwa Intaneti, ambayo mara nyingine huitwa jukwaa la mtandao, ni jukwaa la kweli la kubadilishana na kupata mawazo, ushauri na uzoefu. Mawasiliano ya jukwaani ni solandanifu, yaani maswali/maombi hayajibiwi moja kwa moja na kwa mfulululizo lakini yanachukua masaa, siku au hata majuma. Faida yake ni kwamba watu kutoka sehemu zao mbalimbali wanaweza wakachagua muda mwafaka kuandika au kujibu swali ambalo ni la msaada hasa pale linapovuka kanda mbalimbali za muda. Kwa kawaida jukwaa kwa mtandao linakuwa na ujumbe maalum na linatoa maelekezo mbalimbali au majukwaa madogo kwa mada ndogo. Unaweza ukaandika "ujumbe" ambao unaweza kusomwa na kujibiwa na watu wengine. Michango yote inayounganishwa na ujumbe maalumu unaitwa mlolongo wa mawazo au mada kwa kuanza habari mpya unaanzisha majadiliano mapya.[16] Hii inarahisisha kuweka mpangilio wa mada kuliko mawasiliano ya barua pepe. Uwezekano mwingine ni wakubadilishana nyaraka, picha au video mapitio au ushauri wa baadhi ya mambo, n.k. kwa hiyo, jukwaa la mtandao ni chombo imara kwa mawasiliano ya kisasa na kinatumika sana kwa makundi au jumuiya ambazo zinapenda kuwasiliana nje ya kanda za muda au umbali wa kijografia. Neno la siri linaiificha kwa wasiohusika ili iweze kutumika tu na wanachama waliothibitishwa.

Blogi: ni kwa ajili ya kubadilishana makala, fikra, sala n.k. Chombo hiki kinaruhusu kundi au jumuiya kushirikishana maandiko ya kiroho na tafakari pamoja na kuweka picha, video fupi na jalada la sauti. Hata hivyo blogi inafanana sana na kitabu cha kumbukumbu au jarida, inaweza ikaandikwa na kuhariri wa na watu mbalimbali. Zana za kutafsiria inawezesha kuwasiliana kwa lugha mbalimbali. Baadhi ya vituo hivi tayari vimeshafikiriwa kuwa machapisho ya mtandao na zimepewa namba za ISS.[17]

Simu za Kuona: ni kupiga simu na kuona sura kama simu za kuonea. Skaipu na simu ya waonaji ni programu nyingine za komputa zinazofaa kama hizi. Kwa simu ya waonaji watu kadhaa wanaweza kufanyia kazi dokumenti moja kwa pamoja hata kuvuka mabara. Na kunakuwa hakuna wasiwasi kwamba kuonana moja kwa moja ni faida ya nyongeza.

Fursa zote hizi inafungua mipaka mipya na nafasi mbalimbali ambazo zilikuwa zinatumika na mashirika mbalimbali ya kitawa.[j] Katika familia ya Kisalvatoriani njia hizi ndio kwanza zinaanza kutumika. Katika Injili ya Matayo 11:17 tunasoma: "Tulicheza tulipiga filimbi kwa ajili yenu, lakini hamkucheza, tuliimba kwa huzuni, lakini hamkulia;" Kwa bahati mbaya, jambo hili linaweza kutumika hapa. Kwa sasa, hii tunayoita mitandao ya kijamii kama vile Face Book, tuita na Co. inapata watumiaji mbalimbali, majukwaa na blogi vimetumiwa sana au kidogo, ingawa

[j] Shirika la watawa wa jamii ya Maria huwa wanatumia njia ya "jumuiya ya mtandao" kwa muda mrefu.

mawasiliano yanafanyika kwa kujificha na inatoa usalama mdogo. Ushawishi mkubwa unahitajika na uelewa wa jumuiya za mtandao ambazo wana haki na wajibu.

Hitimisho

Tumeona kwamba jumuiya inaweza kugawanyika katika hatua nne kutokana na kiwango cha uhakika. Inahusisha ujasiri, uvumilivu na pia kupitia vikwazo mbalimbali katika hatua tatu za kwanza kiwango cha jumuiya ya kweli hakiwezi kufikiwa mpaka kuwa na upendo usio wa masharti ambao Baba Jordani aliuonyesha katika kitabu chake cha kiroho:

"Wengine watavutiwa kujiunga na jumuiya yetu kama wataona upendo umeenea kati yetu."

Hili ni lengo linalostahili na dhumuni ambalo linaweza kufikiwa endapo wanachama wataelewa wito wao na kutumia vipaji vyao kwa faida ya wote. Mipaka, bahari na Mabara yanazidi kuwa karibu sana katika muda wetu. Umbali unapungua na vyombo vya habari vinafungua fursa mpya. Wajibu wetu sasa ni kujihusisha na kuvitumia kwa faida na Baraka kwa wote. Na hii inaweza ikatusaidia kufikia kile kinachosemwa na Wafilipi 1:27a

"Kama jumuiya ishini kwa namna inayoendana na Injili."

Maswali ya Tafakari

1. Soma tena Sheria za Familia ya Kisalvatoriani kwa mwanga wa makala hii.
    a. Onyesha maneno au misemo ambayo inakugusa na ujiulize, "jambo hili linaniambia mimi nini na nitalipa mwitikio gani?"
    b. Manufaa yake yanaweza kuwa ni yapi katika familia ya Kisalvatoriani katika eneo lako la ulimwengu au/na kwa ulimwengu mzima?
2. Kwa mwanga wa makala hii, kama ukiamua kuitengeneza upya sheria ya familia ya Wasalvatoriani, Je, Utaongeza kitu gani au kukibadili?

Bibliograpy

1
2
3
4
5
6
7
8
9
10
11
12
13
14
15
16
17